# Kutumia Wakalimali kwa ajili ya Mawasiliano na Shule

Huko Ohio, shule na familia hushirikiana ili wasaidie watoto kufaulu. Huwa wanafanya hivyo kwa kuzungumza na kushiriki taarifa muhimu wao kwa wao Lazima shule zishiriki taarifa katika lugha ambazo familia zinapendelea. Familia yako inaweza kusaidiwa na wakalimani kuuliza maswali na kushiriki mawazo au wasiwasi wenu na shule.

## Ukalimani na Tafsiri

### Je, wakalimani ni akina nani?

Wakalimani ni wataalamu ambao husaidia watu wanaozungumza lugha tofauti kuwasiliana. Huwa wanamsikiliza mtu mmoja akizungumza kwa lugha moja. Kisha wanashiriki taarifa hiyo na mtu wengine kwa lugha tofauti. Wakalimani wanaweza pia kusaidia kuelezea tofauti za kitamaduni. Wafikirie kama daraja la kuelewa mwalimu wa mtoto wako.

> Mkalimani anaweza kusaidia familia inayozungumza Kisomali kuwasiliana na mwalimu wa mtoto wao anayezungumza Kiingereza. Mkalimani anaweza kumwambia mwalimu kwa Kiingereza kuhusu mambo ambayo mzazi au mlezi anasema. Kisha anaweza kumwambia mzazi au mlezi kwa Kisomali kuhusu mambo ambayo mwalimu anasema.

### Aina za Wakalimani

- Wakalimani wa ana kwa ana hukuwa katika sehemu moja na familia na huwa wanafasiri ana kwa ana. Wakalimani wa simu hufasiri moja kwa moja kupitia simu.
- Wakalimani wa video huwasiliana kupitia video. Huwa wanatumia kifaa kama vile simu janja au kompyuta.
- Wakalimani wa Lugha ya Ishara hutoa huduma ya kutafsiri kwa watu walio na matatizo ya kusikia. Baadhi ya watu hupendelea kuwasiliana kupitia lugha ya

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

ishara. Wakalimani wengi wa lugha ya ishara wamefundishwa kuhusu msamiati wa Lugha ya Ishara ya Marekani. Huenda lugha hii ya ishara isifanane katika tamaduni na lugha nyingine.

## Je, nani anaweza kuwa mkalimani?

Lazima wakalimani wapate mafunzo na wathibitishwe. Ukalimani unahitaji ujuzi na mafunzo maalum. Shule hazipaswi kutegemea wanafunzi, ndugu, au watu wazima wasio na mafunzo ili wawe wakalimani.

Watoto wanaotoa huduma ya ukalimani kwa wazazi wao wanaweza kuwa na mfadhaiko au shinikizo kubwa. Jambo hili ni kweli hasa ikiwa mazungumzo yanajumuisha maneno au mada ambazo hawajui. Unapotumia mtu ambaye hajafundishwa kama mkalimani, kuna hatari kubwa ya kutokuelewana kati ya shule na familia. Hii ni kwa sababu huenda akakosa kuelewa michakato ya elimu, mifumo au maneno yote yanayotumiwa na shule.

### Je, tafsiri ni nini?

Tafsiri ni wakati taarifa imeandikwa kutoka lugha moja hadi nyingine. Mtu aliyefundishwa kufanya kazi hii anaitwa mtafsiri. Baadhi ya mashirika ya kijamii hutoa huduma za kutafsiri bure au kwa bei nafuu.

## Je, shule ina jukumu gani katika kutoa huduma za ukalimani na tafsiri?

- Huko Ohio, lazima shule zitafsiri nyenzo zilizoandikwa.
  Shule zinaweza kuomba familia zilete nakala za shule zilizotafsiriwa wanapomwandikisha mtoto wao katika shule mpya. Katika hali hizi, huenda ukahitaji kulipa ada ili upate nakala zilizotafsiriwa. Baadhi ya mashirika ya jamii yanaweza kutoa huduma za kutafsiri kwa gharama ya chini au bure.
- Shule lazima zitoe wakalimani na huduma ya tafsiri bure kwa familia zinazoomba huduma hizo.

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University 

- Lazima mkalimani aheshimu faragha ya familia.
- Shule zinapaswa kuhakikisha kuwa wakalimani wanafundishwa kusaidia katika mazingira ya elimu.

## Je, wakalimani wanaweza kusaidia wakati gani?

Unaweza kuomba msaada kutoka kwa mkalimani wakati wowote unapohitaji kuzungumza na mtu katika shule ya mtoto wako. Huduma hii inaweza kukusaidia unapokutana na mwalimu wa mtoto wako au wafanyakazi wengine.

### Kuna baadhi ya mifano hapa:

- Mikutano ya Wazazi na Walimu
- Mikutano kuhusu mahitaji ya elimu maalum ya mtoto wako
- Mikutano ya mshauri nasaha wa shule
- Ziara za nyumbani: wafanyakazi wa shule wanapokutembelea nyumbani ili wajue familia yako
- Matukio ya shule kwa ajili ya familia
- Mikutano ya bodi ya shule: mikutano ambapo maamuzi hufanywa kuhusu sera za shule na mambo mengine muhimu yanayoathiri wanafunzi, familia, na shule

## Je, ninaweza kuomba huduma za mkalimani vipi?

Mkutano unapopangwa shuleni, unaweza kumwambia mtu anayepanga mkutano kwamba unahitaji mkalimani. Ni muhimu kutoa ombi hili haraka iwezekanavyo. Ukifanya hivyo, shule itapata muda wa kupata mkalimani.

Kuna watu wengine katika shule ambao wanaweza pia kukusaidia kuomba huduma za mkalimani kama vile:

- Mwalimu wa lugha ya Kiingereza
- Mwasiliani wa familia
- Mshauri nasaha wa shule

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University 

- Mwalimu wa mtoto wako
- Msaidizi wa ofisi au katibu

## Maswali Unayoweza Kuuliza kuhusu Wakalimani

Hapa kuna orodha ya maswali unayoweza kuuliza unapoomba huduma za mkalimani:

- Je, mtoto wangu, mwanafamilia, au rafiki yangu anaweza kunifasiria?
- Ninaombaje huduma za mkalimani kwa ajili ya mikutano ya shule?
- Je, kuna mchakato maalum au fomu ninayohitaji kujaza ili kuhakikisha kuwa mkalimani atakuwepo katika hafla za shule?
- Je, ikiwa ninahitaji mkalimani, ninapaswa kuomba huduma za mkalimani lini?
- Nitajuaje ikiwa mkalimani ataheshimu faragha yangu na kuwa hatashiriki taarifa yoyote na watu wengine?
- Ninawezaje kutoa maoni kuhusu ubora wa huduma za tafsiri ninazopokea?

## Vidokezo kwa Wazazi Wanaotumia Mkalimani

1. Tenga muda wa ziada kwa ajili ya mikutano au matukio yanayojumuisha mkalimani. Mara nyingi, kuwasiliana na mkalimani huchukua muda wa ziada.
2. Unapozungumza, mtazame mtu unayekutana naye machoni. Usimtazame mkalimani. Kufanya hivi huruhusu mtu huyo mwingine aone ishara zako zozote. Kufanya hivi kunaweza kukusaidia kuelewa vizuri zaidi.
3. Mkalimani yupo hapo ili akusaidie kuwasiliana na shule.
4. Huenda ukaona kana kwamba mkalimani anakupuuza au kwamba anachukulia mambo kwa uzito sana. Huenda anazingatia tu kusaidia kila mtu kuelewana.
5. Wakalimani lazima waheshimu faragha ya familia. Hawaruhusiwi kuwaambia watu wengine kuhusu mambo ambayo familia zinashiriki na shule.
6. Jaribu kuzungumza kwa sentensi moja au mbili fupi kwa wakati mmoja. Ni

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

muhimu kuzingatia kushiriki mawazo kamili. Kisha, pumzika ili umpe mkalimani muda wa kushiriki mambo yanayosemwa.

7. Mkalimani anaweza kuinua mkono wake au kutoa ishara tofauti. Hii inamaanisha kuwa anakuhitaji wewe au mtu mwingine mwache kuongea kwa muda.
8. Ikiwa jambo lolote halijaeleweka, mkalimani anaweza kukuomba uliseme tena.
9. Ni muhimu kukumbuka kwamba wakati mwingine, huenda tafsiri za kitamaduni zisieleweke vizuri kabisa, kama vile ishara za mkono au misemo ya kimazungumzo.

## Rasilimali za Ziada

- Ukurasa wa Kukuza Mawasiliano Mazuri Kati ya Mzazi au Mlezi na Mwalimu kutoka katika Chuo Kikuu cha Minnesota (University of Minnesota) hutoa taarifa zaidi kuhusu jinsi ya kushirikiana na mkalimani katika lugha mbalimbali. Unaweza kusikiliza au kusoma taarifa hiyo. https://publications.ici.umn.edu/nceo/improving-instruction-parent- educator-toolkit/building-successful-communication-between-parent-or-guardian-and-teacher
- Jifunze zaidi kuhusu kushirikiana na Wakalimani wa Lugha kwenye tovuti ya Chuo Kikuu cha Minnesota (University of Minnesota). Ina taarifa katika Kiingereza, Kiarabu, Kichina Kilichorahisishwa na Sanifu, na Kivietinamu. https://publications.ici.umn.edu/nceo/improving-instruction-parent-educator-toolkit/working-with- language-interpreters
- USA Hello hutoa rasilimali kwa familia kuhusu ukalimani, tafsiri, na mada nyingine muhimu kuhusu elimu. https://usahello.org/education
- Taarifa kwa Wazazi Wenye Ujuzi Mdogo wa Kiingereza na kwa Shule na Wilaya za Shule zinazowasiliana nao kutoka Colorin Colorado ni hati ya kuarifu inayopatikana katika lugha nyingi. Inajibu maswali ya kawaida kuhusu haki za

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University

wazazi na walezi wasioweza kuzungumza, kusikiliza, kusoma, au kuandika Kiingereza kwa ufasaha kwa sababu si lugha yao ya msingi. https://www.colorincolorado.org/guide/fact-sheet- information-limited-english-proficient-parents-and-schools-and-school-districts

## Programu za Simu ya Mkononi

- Google Lens hukuwezesha kutumia simu yako kutafsiri maneno kwa kuchanganua tu matini kwa kamera yako au kutumia picha. Unaweza kutafuta kile unachokiona, kufanya mambo haraka na kuelewa mazingira yako.

*Rasilimali hizi zinalenga kuimarisha masomo, ustawi wa wanafunzi, na matokeo ya chuo na kazi kwa wanafunzi wa Ohio wanaozungumza lugha nyingi. Rasilimali ziliundwa kupitia juhudi za kushirikiana kati ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (Ohio Department of Education and Workforce) na Kituo cha Chuo Kikuu cha Jimbo la Ohio cha Elimu na Mafunzo ya Kazi (The Ohio State University's Center on Education and Training for Employment) pamoja na kikundi cha kujitolea cha watetezi wa familia, viongozi wa jamii, wafanyakazi wa wilaya ya shule, na walimu.*

[Copyright] ©2024 Center on Education and Training for Employment, The Ohio State University